**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

MKOA WA NJOMBE
SIMU 026-2790001
**FAX 026-2790001**

OFISI YA MKUU WA WILAYA
S. L. P. 2
**LUDEWA**

KUMB. NA. AB/127/414/01/80

Tarehe 17/07/2022

# TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI WA NAFASI ZA MAKARANI, WASIMAMAIZI WA MAUDHUI NA WASIMAMIZI WA TEHAMA KWA AJILI YA ZOEZI LA SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022

MWENYEKITI WA KAMATI YA SENSA WILAYA YA LUDEWA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE WALIOOMBA KAZI YA MUDA YA MAKARANI, WASIMAMIZI WA MAUDHUI NA WASIMAMIZI WA TEHAMA KWA AJILI YA ZOEZI LA SENSA YA WATU NA MAKAZI 2022 KUHUDHURIA USAILI UNAOTARAJIA KUFANYIKA KUANZIA TAREHE **19-21/07/2022**

USAILI HUO UTAFANYIKA KATIKA MAKAO MAKUU YA KATA AMBAKO MHUSIKA ALIWASILISHA MAOMBI KATIKA NAFASI ZA MAKARANI NA WASIMAMIZI WA MAUDHUI

KWA WALE WALIOOMBA NAFASI YA USIMAMIZI WA TEHAMA, USAILI UTAFANYIKA KATIKA MAKAO MAKUU YA WILAYA (LUDEWA).

AIDHA, WAOMBAJI WOTE WA NAFASI HIZO WANATAKIWA KUWA NA VITU VIFUATAVYO:

1. VYETI VYOTE VYA TAALUMA (ORIGINAL CERTIFICATES) NA NAKALA ZAKE.

Scanned with CamScanner

2. VIAMBATISHO VINGINE ULIVYOAMBATISHA ( UJE NA ORIGINAL NA COPY YAKE)
3. NAKALA YA FOMU NA .1 ILIYOSAINIWA NA AFISA MTENDAJI KATA/KIJIJI WA ENEO HUSIKA
4. VIFAA VYA KUANDIKIA KAMA KALAMU YA RISASI, PENI, KARATASI NYEUPE 3 .

MUDA WA KUANZA USAILI NI SAA 2:00 ASUBUHI, HIVYO WAOMBAJI WOTE MNATAKIWA KUFIKA MAPEMA. KUMBUKA UKICHELEWA HAUTARUHUSIWA KUINGIA KWENYE USAILI.

MAJINA YA WAOMBAJI UNAWEZA KUYAPATA SEHEMU ZIFUATAZO: MBAO ZA MATANGAZO ZA OFISI ZA KATA, KWENYE TOVUTI YA HALMASHAURI NA KWENYE UBAO WA MATANGAZO WA HALMASHAURI.

**N.B**

**MAAFISA WATENDAJI WA KATA NA VIJIJI HAWARUHUSIWI KUWA MAKARANI, WASIMAMIZI WA MAHUDHUI NA WASIMAMIZI WA TEHAMA KATIKA NAFASI ZILIZOTANGAZWA ILA WATAKUWA NA MAJUKUMU MENGINE KATIKA SHUGHULI ZA SENSA.**

NAWATAKIA USAILI MWEMA.

SUNDAY N. DEOGRATIUS
K.N. Y MWENYEKITI WA KAMATI YA SENSA
**WILAYA YA LUDEWA**

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
Ludewa

TANZANIA
SENSA
23 Agosti
2022
Jiandae Kuhesabiwa

Scanned with CamScanner